**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI**

**Namba za Simu 0716570609 Mhasibu wa shule** **S. L . P 75**

**Mkuu wa Shule 0786036520/0620616680** **IKWIRIRI/RUFIJI**

**Makamu Mkuu wa Shule 0718849885** **TAREHE …………………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………...................................**

**S.L.P ….......**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI HALMASHAURI YA WILAYA YA MJI RUFIJI MKOA WA PWANI**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …….. na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Ikwiriri ipo mkoa wa Pwani, Wilaya ya Rufiji umbali wa Kilometa 160 Kutoka Jiji la Dar es Salaam. Kwa wanafunzi wanaotoka mikoani wafike Stendi ya Mabasi Mbagala Rangi tatu jijini DSM ndipo watapata Usafiri wa basi kutoka jijini DSM hadi Ikwiriri stendi kwa nauli ya 9,000/= na wanafunzi wanaotoka Mikoa ya Lindi na Mtwara washukie Ikwiriri stendi. Ukifika Stendi Ikwiriri utaletwa hadi shuleni kwa usafiri wa pikipiki kwa nauli ya Shilingi 1500/=.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe………. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……….

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii kwa Wasichana ni sketi mbili rangi ya orange mshono wa linda box yenye urefu hadi chini iguse viatu.
ii. Mashati rangi nyeupe mawili ya mikono mirefu au/nusu kanzu mbili kitambaa cha harua kwa wanaovaa hijab
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni rangi nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iv. Sare ya Michezo ni trucksuits moja rangi ya blue Iliyokoza rangi yake (truck suit iwe na nembo ya shule) Kwa wasichana na raba rangi nyeupe
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe
vii. Sweta moja rangi ya bluu
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) sketi rangi ya kijani mshono wa linda box na juba rangi nyeupe au pink kwa wanaovaa hijab
ix.T-shirt yenye nembo ya shule moja au zaidi kwa ajili ya kuvaa darasani kwa siku maalum na masomo ya jioni.
x.Jezi yenye nembo ya shule moja kwa ajili ya kushindia.
xi. sketi ya kijani iliyokoza moja mshono wa linda box yenye urefu hadi chini iguse viatu utaishona nyumbani na utavaa siku ya kuja kuripoti shuleni

**ANGALIZO: Sketi za shule rangi ya orange na kijani unaweza kushonewa na mafundi walioko karibu na shule ili kukurahisishia upatikanaji wa vitambaa vyenye mfanano wa rangi na urefu unaotakiwa ili kuepusha kutofautiana rangi**. **Ukishona kitambaa kilichotofauti na wenzako utapata hasara ya kushona nyingine**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa 08 (counter book 3 quire)
ii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha ime ambatishwa*);
iv. Scientific Calculator na graph pad moja kwa wanaosoma Geography
v. Godoro la futi2.5 kwa 6

vi. Mashuka rangi ya sky blue Jozi 2, foronya ya godoro 1, chandarua rangi nyeupe kimoja
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Kandambili(bata/bora) kwa ajili ya kuogea na sandal za kimasai zisizo na urembo kwa ajili ya kushindia.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe, hotpot moja na chupa ya chai moja);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko ;
xi. Sanduku imara la bati moja lenye makufuli mawili(tranker)
xii. Photocopy za cheti cha kidato cha nne na cheti cha kuzaliwa.
xiii. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na fagio la wima la chelewa lenye mpini
xiv. Sabuni ya maji lita moja na nusu

**ANGALIZO**: **Mwanafunzi anaweza kununua vitu hivi katika mji wa Ikwiriri kukwepa gharama za usafiri kwa wanafunzi wanaotoka mikoa ya mbali**.
**Kila mwanafunzi anatakiwa kufungua akaunti yake binafsi ya benki CRDB au NMB kwa ajili ya kutunza fedha zake za nauli na mahitaji yake madogo madogo ukija shule utaelekezwa namna ya kufungua,uje na picha za passport size mbili. Pia unatakiwa kuwa na Bima ya Afya CHF au NHIF**

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Michango yote ya shule inayolipwa Benki.**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote ya shule inalipwa kwenye akaunti ya Benki ya NMB namba 21301100032 Jina la akaunti ni IKWIRIRI SECONDARY SCHOOL RECCURENT EXPENSES. Jina la mwekaji pesa liwe jina la mwanafunzi na si vinginevyo**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI

yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule, unatakiwa kuwa na nywele fupi za kuchana na kitana kidogo kwani haturuhusu kusuka nywele;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.
xii. Huruhusiwi kufanya sherehe yoyote ile eneo la shule bila kibali cha mkuu wa shule.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- ❖ **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu au meneno ya uchonganishi kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kutoroka kwenda nje ya mipaka ya shule , kukaa au kupita maeneo na njia zisizoruhusiwa;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba au kusababisha mimba;
xii. Kukwepa kazi za shule,vipindi vya masomo na kujificha mahali pasipo julikana;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu au sehemu ya simu ya mkononi kama vile laini ,charger, earphone,headphone,memory card ,tablet ipad na smartwatch katika mazingira ya shule;
xvi. Kuvuruga amani na usalama watu katika mazingira ya shule.
xvii. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa taifa;
xviii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xix. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xx. Kufanya mikusanyiko na mikutano shuleni bila kibali cha mkuu wa shule au uongozi wa shule.
xxi. Kumiliki vifaa vyenye ncha kali bwenini

OR – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA RUFIJI

SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI

MKUU WA SHULE: +255786036520/+255620616680 .

MAKAMU: +255718849885

MHASIBU: +255716570609/+255752787083 S. L . P 75

I IKWIRIRI/RUFIJI

## MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

**MWANAFUNZI**

Jina la mwanafunzi……………………….……………adm.Na……………

Kidato …………………mchepuo…….…………mwaka…………

Tarehe ya kuzaliwa………………… Mahali ulipozaliwa…………………

Kabila la mwanafunzi………………………… Uraia wa mwanafunzi…………………

Tarehe ya kujiunga na shule ya sekondari ya Ikwiriri…………Shule aliyotoka ya sekondari……

Masomo utakayokuja kusoma………… Kama ni mlemavu,taja aina ya ulemavu………………

Je unarudia kidato?……… kwa nini?.........................................

Dini ya mwanafunzi………………Dhehebu………………………

Anwani ya kudumu ya mwanafunzi S.L. P…
Wilaya………Mkoa………………Tarafa…………Kata………………..
Kijiji…………………Namba ya nyumba……………… Simu nyumbani……… Simu ya ofisini…………

**BABA**

Jina la Baba…………………………. Je,yu hai ?………

Kabila la baba…………………Anwani yake ya sasa………………Kazi yake…………… Mwajiri wake………………

Dini ya baba ………………….dhehebu………

Je,baba na mama wanaishi pamoja?............................ Simu ya baba………Ya kazini……………

**MAMA**

Jina la mama…………………………………

Je,yu hai?........................ Kabila la mama……………

Mwajiri wake …………………………

Anwani yake ya sasa……………………

Dini ya mama…………………Dhehebu…………………

Kazi yake ………………mwajili wake………………

Simu ya nyumbani……………Ya ofisini…………

**MLEZI**

Jina la mlezi…………………… Kabila la mlezi……………………

Uhusiano na mwanafunzi ukoje?............................. Anwani ya sasa……………

Kazi yake…………………Mwajiri wake…… Dini ya mlezi………………Dhehebu………………

Simu ya nyumbani…………Ya kazini……………

| PICHA -BABA | PICHA-MAMA | PICHA-NDUGU WA KARIBU | PICHA-NDUGU WA KARIBU |
|---|---|---|---|
| | | | |

**Sahihi ya mwanafunzi……………** **Tarehe…………………**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART 'A'

FROM………………………

TO THE MEDICAL OFFICER ……………………………… ……….
Mr./Miss……………………………………………(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full – time student. The examination should include the following categories (I – III) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case of a defect. Pregnancy (category IV) will also render a girl student ineligible for studies.

I (a) Eyesight (e) Venereal Diseases (b) Hearing (f) Leprosy (c) Speech (g) Epilepsy
(d) Limbs

II Neuroses

III Other serious diseases

Date……………………… Signature……………………

PART B:

## MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above – named and consider that he/she is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full – time student.

I (a) Eyesight…………………… (e) Venereal Diseases…………………

(b) Hearing……………………. (f) Leprosy………………………….

(c) Speech ……………………. (d) Limbs………………………

II Neuroses…………………………………………

III Other serious diseases…………………………

IV. Pregnancy……………………………………

Date……………………………………………Signature……………………………........
Station……………………………………... Designation………………………………

## E. AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………… Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI IKWIRIRI KIDATO CHA TANO Mchepuo wa ………… mwaka …… ninaipokea na kuikubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa na Shule ya Sekondari ya Bweni Ikwiriri.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

i. Nitasoma Kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo niliyo changuliwa kusoma
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu. ……………………………………(Jina la mzazi) Kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi …………………… Tarehe …………………………………

**SEHEMU YA MZAZI/MLEZI**

Mimi …………………………………………… ninakubali mtoto wangu …………………… Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari ikwiriri mwaka ….. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa. Anuani yangu ya kudumu ni …………………………… Simu …………………. Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini ya Mazazi/Mlezi ………………………Tarehe ………………………….

## F.VITABU

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na baadhi ya vitabu kutokana na masomo (Mchepuo) anayokuja kusoma hapa shuleni.Mwanafunzi atakaguliwa vitabu hivi mara tu atakapofika shuleni

1. GENERAL STUDIES
   Kila mwanafunzi lazima aje na kitabu cha somo la General studies kati ya General studies for A' LEVEL Written By
   Joannes Bigirwamungu & Sospeter M. Deogratus
2. GEOGRAPHY
   Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kusoma somo la Geography anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya
   - Physical Geography by Monk House
   - Practical Geography for Africa By John Richard
   - Fundamental Geography By Josephat

3. HISTORY
   Kila mwanafunzi anayekuja kusoma somo la History anatakiwa kuja na vitabu japo viwili kati ya
   - Essential in Advanced level History paper 1 By Saleh Yassin
   - Advanced Level history Paper 1 By Zisti Kamili
   - The Evolving World By Denis Ngalula
   - Advanced level History Paper Two By Pascrates Fidelis Rutta

4. ENGLISH LANGUAGE
   Kila mwanafunzi aliyechaguliwa kuja kusoma somo English Language anatakiwa kuja na vitabu viwili kati ya
   - Advanced English Oxford Dictionary 7th Edition (Lazima aje nayo)
   - Introduction to literature by Chace .W.M & Collier
   - Essential English language two second edition by Filbert Kabila & JULIUS Mombeki
   - English language One Form five & six By Kadeghe M
   - English for Advanced Secondary Schools Student's Book Form Five; (2022) Tanzania Institute of Education

***NB;*** *mwanafunzi anatakiwa pia kuja na angalau vitabu viwili vya PLAY,vitabu na vitabu Viwili vya*

*NOVELS*

**NOVELS**

- Chasing the leopard finding the lion (Julie Wakeman-linn)
- The opportunist elite (Nyambari Nyangwine)
- The Horizon unveiled ( Fellowes Mwaisela)
- Animal Farm ( George Orwell)

**PLAY**

- The government Inspector (Nicolai V. Gogol )
- An Enemy of the people ( Henrik Ibsen)
- A Taste of Heaven (Farouk Topan)

POETRY

- Summons; Poems from Tanzania (Richard .S. Mabara et al.)
- Poets of Africa; Lament of the Silent and other poems ( Jared Angira)

12. KISWAHILI

Kila mwanafunzi aliyepangwa kuja kusoma somo la Kiswahili anatakiwa kuja angalau na vitabu viwili kati ya

- Kiswahili kidato cha 5 na 6 kiswahili 1 Lugha na Sarufi (Taasisi ya Elimu Tanzania) 2019
- Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili 2 (Kilangi Enock LUCAS)
- Tafsiri na Ukalimani (Mwansoko)
- Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI) Lazima aje nayo Vile vile mwanafunzi anayesoma Kiswahili anapaswa kuja na vitabu vya RIWAYA viwili,MASHAIRI viwili na TAMTHLIYA viwili (**Chagua hapo chini kwenye orodha)**

**USHAIRI**

- Fumbo linaloelea (Nyambari Nyangwine)
- Malenga wa ziwa kuu (Wallah Bin Wallah)
- Andamo msafiri safarini (Mohamed Khelef Ghassani)
- Wosia wa Baba ( Ahmed Mohamed Amanzy)

**RIWAYA**

- Dunia uwanja wa fujo (E. Kezilahabi)
- Ua la faraja (W . E. Mkufya)
- Mirathi ya hatari ( C.G. Mung'ong'o)
- Wasifu wa siti Binti saad (Shabani Robert)

**TAMTHILIYA**

- Mukwava wa Uhehe (M . M . Mulokozi)
- Shujaa Mirambo ( Emmanuel Mbogo)
- Usaliti Mjini (Francis Imbuga)

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………**
**Jina la Mkuu wa Shule NURU SALUM MNIKU**
**Muhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0786036520/0620616680**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0718849885**